# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## VETA

## CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA VETA TABORA

MKATABA WA FUNDI UJENZI

**1.0 Maelezo ya mkataba**

i) Jina la mkataba: - KAZI ZA UMALIZIAJI JENGO LA UTAWALA.

ii) Na. ya mkataba: VETA/TBR/UYUI/DVTC/PHASE II/ADMIN/BLOCK/09.

**2.0 Makubaliano:**

Makubaliano haya yamefanyika leo siku ya ALHAMIS.........Tarehe ....24......... mwezi .....MACHI..... Mwaka ......2022.............. Kati ya Mkuu wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma VETA Tabora (Tabora RVTSC) wa S. L. P. ......2060...... Tabora, ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 Dodoma (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

Misayo Bernard Nawita wa S. L. P. 728, Tabora (ambaye hapa anatambulika kama Fundi).

Kwamba mwajiri anampatia Fundi kazi ya umaliziaji katika jengo la utawala kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Kuweka rough floor na skirting | Tsh | 4,286,000.00 |
| ii. | Skimming | Tsh | 1,350,000.00 |
| iii. | Kupaka rangi na varnish | Tsh | 750,000.00 |
| iv. | Blundering na kufunga board | Tsh | 1,014,000.00 |
| v. | Kufunga Milango | Tsh | 450,000.00 |
| vi. | Kufunga gutters | Tsh | 450,000.00 |
| vii. | Ramp finishing | Tsh | 700,000.00 |
| | **Jumla** | **Tsh.** | **9,000,000.00** |

Kwamba kazi hizi zitafanyika katika eneo la chuo cha Ufundi cha Wilaya ya Uyui lililopo eneo la Idete mkabala na shule ya sekondari ya Idete, Wilaya ya Uyui katika mkoa wa Tabora.

Gharama ya kazi hizi zote ni jumla ya **Shilingi 9,000,000.00** Kwa **maneno, (Shilingi Milioni Tisa Tu).**

Kwamba kazi hizi zitachukua muda wa siku 22 kwa maneno ( Ishirini na mbili ) mpaka kukamilika.

**3.0 Mwajiri:**

Kwamba mwajiri amekubali gharama zilizotolewa na Fundi kwa kazi zilizotajwa hapo juu.

**4.0 Fundi:**

Fundi amekubali kuzifanya kazi hizo za ujenzi kwa kusimamiwa na Wasimamizi wa ujenzi pamoja na kamati ya ujenzi kwa gharama zilizoelezwa hapo juu na kuikamilisha kwa siku zilizotajwa hapo juu.

**5.0 Mwajiri na Fundi kwa pamoja wamekubaliana:**

i Kwamba kazi zitafanyika kwa kiwango cha hali ya juu kwa mujibu wa viwango vya majengo ya serikali.

ii Kwamba kabla ya malipo kazi zitakaguliwa na Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui aliyeteuliwa kukagua kazi za ujenzi wa chuo cha ufundi Uyui.

iii Kwamba Fundi hataendelea na hatua nyingine ya ujenzi mpaka hatua ya awali imekaguliwa na kukubalika na Mhandisi wa Wilaya na kamati ya ujenzi.

iv Kwamba iwapo itabainika kwamba Fundi amejenga kinyume na maelekezo ya Msimamizi wa ujenzi, Fundi atawajibika kubomoa na kurekebisha kwa gharama zake.

vi Kwamba malipo yatalipwa pale tu ambapo awamu husika ya ujenzi imekamilika na imekaguliwa na Mhandisi wa Wilaya ya Uyui pamoja na kamati ya ujenzi na kuthibitishwa kwa maandishi.

vii Kwamba malipo yote yatafanywa kupitia mfumo wa malipo serikalini (MUSE) kwa hiyo Fundi anatakiwa kuwa na akaunti benki.

viii Kwamba endapo itabainika kuwa Fundi anakiuka masharití ya mkataba huu bila sababu za msingi,uongozi wa chuo cha ufundi VETA Tabora utafuta/utavunja mkataba huu na Fundi hatalipwa chochote na hatua za kisheria zitachukuliwa.

**7.0 Fedha ya zuio (retention fund)**

Mwishoni mwa kazi iliyoanishwa katika Mkataba huu, Mwajiri atabaki na 5% ya gharama ya ujenzi hadi pale muda wa matazamio ya ujenzi (miezi sita) utakapokwisha. Fedha hizo zinaweza kutumika pale tu ambapo kuna uharibifu umetokea katika ujenzi ndani ya kipindi cha matazamio ya ujenzi na Fundi akashindwa au akakataa kurekebisha uharibifu huo ndani ya muda wa majuma mawili (2) baada ya kupata maelekezo ya Mwajiri.

**8.0 Nyaraka zinazokamilisha mkataba huu ni:**

- Hati za bei za Fundi
- Michoro na vipimo vya majengo
- Barua ya kukubali kazi ya Fundi
- Mkataba wenyewe
- Orodha ya kazi zitakazofanywa zimeambatanishwa.

**9.0 Saini za pande zote mbili:**

Imetiwa saini na

**MWAJIRI**

Jina: DKT. KYOMO, Z. B.

Cheo: MKUU WA CHUO

Saini: ..............................

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UFUNDI NA HUDUMA
TABORA

**SHAHIDI**

Jina: JAPHARY B. MUSAMBEE

Cheo: HRAO

Saini: ..............................

**FUNDI**

Jina: MISAYO B. NAWITA

Saini: ..............................

**SHAHIDI**

Jina: Erick J. Nkya

Saini: ..............................

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
## VETA
## CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA VETA TABORA

MKATABA WA FUNDI UJENZI
(NYONGEZA YA MKATABA)

**1.0 Maelezoyamkataba**

**HiininyongezayaMkataba**

i) **Jina la mkataba:** - KAZI YA BOMBA JENGO LA UTAWALA

ii) **Na. yamkataba:** VETA/TBR/UYUI/DVTC/CONSTRUCTION/ADMN BLOCK/07

**2.0 Makubaliano:**

Makubaliano haya ya nyongeza ya mkataba yamefanyika leo siku ya JUMATATU Tarehe 14 mwezi MACHI Mwaka 2022 Kati ya Mkuu wa chuo cha ufundi na huduma VETA Tabora (Tabora RVTSC) wa S. L. P. 2060 Tabora. (ambaye hapa anatambulika kama Mwajiri)

NA

Bw**Misayo B. Nawita**wa S. L. P. 726 TABORA (ambaye hapa anatambulika kama Fundi).

Katika mkataba huu zimeongezwa kazi za kuweka mfumo wa maji safi na maji taka kwa jingo lote la utawala kwa gharama ya**Tsh. 900,000.00(Laki tisa tu)**

Kwamba kazi hizi zitachukua muda wa siku 10 (siku KUMI)

Mashariti na vigezo vya kazi hii ya nyongeza vinabaki kama mkataba Na: VETA/TBR/UYUI/DVTC/ADMIN/BLOCK/CONSTRUCTION/03 unavyosema.

**3.0 Saini zapandezotembili:**

Imetiwasainina

**MWAJIRI**

Jina: DKT. KYOMO, Z. B.

Cheo: MKUU WA CHUO

Saini: ..........................

**SHAHIDI**

Jina: JAPHARY B. MWAMBETE

Cheo: [illegible]

Saini: ..........................

**FUNDI**

Jina: MISAYO B. NASIJA

Saini: ..........................

**SHAHIDI**

Jina: Erick J. Nkya

Saini: ..........................

(47)

Reviewed
Member

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**VETA**

CHUO CHA UFUNDI STADI NA HUDUMA VETA TABORA

FOMU YA MKATABA WA FUNDI UJENZI

**1.0 Maelezo ya mkataba**

i) Jina la mkataba: – MKATABA WA KUJENGA JENGO LA UTAWALA
ii) Na. ya mkataba: VETA/TBR/UYUI/DVTC/ADMIN/BLOCK/CONSTRUCTION/03

**2.0 Makubaliano:**

Makubaliano haya yamefanyika leo siku ya ...IJUMAA...Tarehe ..12...... mwezi ..FEBRUARI...... Mwaka ....2021............... Kati ya Mkuu wa chuo cha ufundi na huduma VETA Tabora (Tabora RVTSC) wa S. L. P. ...2060.............Tabora. (ambaye hapa anatambulika kama Mwajiri)

NA

Bw Misayo Bernard Nawita wa S. L. P. 726, TABORA. (ambaye hapa anatambulika kama Fundi).

Kwamba mwajiri anampatia Fundi kazi ya kujengo jengo la utawala kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | Kubomoa sehemu za marekebisho | Tsh | 500,000.00 |
| ii) | Kujenga nguzo mbili za ndani | Tsh | 250,000.00 |
| iii) | Kujenga nguzo mbili za nje eneo la ramp | Tsh | 150,000.00 |
| iv) | Kurekebisha kuta za vyoo wanawake, kutindua zege, kusuka beam ya chini, kumwaga zege na kujenga kuta mpya, | Tsh | 800,000.00 |
| v) | Kutindua zege sehemu zenye matatizo na kumwaga zege mpya | Tsh | 4,100,000.00 |
| vi) | Ujenzi wa kuta mpya | Tsh | 1,500,000.00 |
| vii) | Kurekekbisha ring beam, kuweka formwork, Na kazi zote za nondo | Tsh | 2,055,000.00 |
| viii) | Kumwaga zege (Beam and Slab) | Tsh | 2,400,000.00 |
| ix) | Kuandaa kenchi na kupandisha | Tsh | 1,800,000.00 |

x) Kupiga bati Tsh 1,500,000.00

xi) Kupachika fremu za madirisha na milango, Tsh 1,550,000.00

xii) Kupiga plaster jengo zima Tsh 3,150,000.00

Kwamba kazi hizi zitafanyika katika eneo la chuo cha Ufundi cha Wilaya ya Uyui lililopo eneo la Idete mkabala na shule ya sekondari ya Idete, Wilaya ya Uyui katika mkoa wa Tabora.

Gharama za kazi hizi zote ni **Shilingi 19,755,000.00** Kwa **maneno Shilingi Milioni Kumi na Tisa Laki Saba Elfu Hamsini na Tano tu**

Kwamba kazi hizi zitachukua muda wa siku ...44..... kwa maneno Arobaini na Nne tu mpaka kukamilika.

**3.0 Mwajiri:**

Kwamba mwajiri amekubali gharama zilizotolewa na Fundi kwa kazi zilizotajwa hapo juu.

**4.0 Fundi:**

Fundi amekubali kuzifanya kazi hizo za ujenzi kwa gharama zilizoelezwa hapo juu na kuzikamilisha kwa siku zilizotajwa hapo juu.

**5.0 Mwajiri na Fundi kwa pamoja wamekubaliana:**

i) Kwamba kazi zitafanyika kwa kiwango cha hali ya juu kwa mujibu wa viwango vya majengo ya serikali.

ii) Kwamba kazi zote zitasimamiwa na msimamizi wa ujenzi pamoja na kamati ya ujenzi waliyoteuliwa na mkuu wa chuo cha VETA Tabora.

iii) Kwamba kazi zitakaguliwa na Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui aliyeteuliwa kukagua kazi za ujenzi wa chuo cha ufundi Uyui.

iv) Kwamba Fundi hataendelea na hatua nyingine ya ujenzi mpaka hatua ya awali imekaguliwa na kukubalika na Mhandisi wa Wilaya na kamati ya ujenzi.

v) Kwamba iwapo itabainika kwamba Fundi amejenga kinyume na maelekezo ya Msimamizi wa ujenzi, Fundi atawajibika kubomoa na kurekebisha kwa gharama zake.

vi) Kwamba kamati ya ujenzi ndio itakayokuwa inatoa na kukadiria kiwango cha kazi na makadirio ya gharama zake.

vii) Kwamba malipo yatalipwa pale tu ambapo awamu husika ya ujenzi imekamilika na imekaguliwa na Msimamizi wa ujenzi, Mhandisi wa Halmashauri pamoja na kamati ya ujenzi na kuthibitishwa kwa maandishi.

viii) Kwamba malipo yote yatafanywa kwa hundi hivyo Fundi anatakiwa awe na akaunti benki.

ix) Kwamba endapo itabainika kuwa Fundi anakiuka masharti ya mkataba huu uongozi wa chuo cha ufundi VETA Tabora utafuta/utavunja mkataba huu na Fundi hatalipwa chochote na hatua za kisheria zitachukuliwa.

x) Malipo yote yatakatwa kodi ya zuio ya asilimia tano (Withholding Tax 5%) kama sheria za kodi zinavyosema.

**6.0 Nyaraka zinazokamilisha mkataba huu ni:**

- Hati za bei za Fundi
- Michoro na vipimo vya majengo
- Barua ya kukubali kazi ya Fundi
- Mkataba wenyewe

**7.0 Saini za pande zote mbili:**
Imetiwa saini na

**MWAJIRI**
Jina: Dkt. Zebedayo Kyomo
Cheo: Mkuu wa chuo
Saini: ........................

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UFUNDI NA HUDUMA
TABORA

**SHAHIDI**
Jina: JAPHARY B. MWAMBEJE
Cheo: HRAM
Saini: ........................

**FUNDI**
Jina: MISAYO B. NAWITA
Saini: ........................

**SHAHIDI**
Jina: Erick J. Nkya
Saini: ........................